



Tennessee Department of Human Services
(Idara ya Huduma za Binadamu ya Tennessee)
Ombi la Usaidizi wa Familia

Tafadhali tuambie ikiwa unahitaji usaidizi wa kuwasilisha ombi hili kutokana na kuwa na ulemavu au kwa kuwa huzungumzi Kiingereza. Usaidizi wa bila malipo upo. Wasiliana na Nambari ya Kituo cha Huduma ya Usaidizi wa Familia kwa 866-311-4287 na/au nambari ya TTY kwa 711. Baada ya ujumbe uliorekodiwa, utamfikia msaidizi ambaye anaweza kukupa mkalimani.

KISANDUKU HIKI NI KWA MATUMIZI YA TDHS PEKEE

ya Kesi: _____
Tarehe ya kupokelewa: _____
Kaunti: _____

Tutachukua ombi lako lenye jina, anwani, na saina yako pekee. Lakini kadiri unavyotupa maelezo zaidi, ndivyo tunavyoweza kuona haraka ikiwa unaweza kupata usaidizi. Ombi lako likidhinishwa, manufaa yako yanaweza kuanza kutolewa kuanzia tarehe tutakayopokea ombi lako. Mara nyingi, utahitaji kuzungumza na mfanyakazi wa TDHS ili kukamilisha mchakato wa kuwasilisha ombi.

Unaweza kupata SNAP ndani ya siku 7 ikiwa:

1. Mapato ya kila mwezi ya kaya yako ni chini ya dola 150, na una rasilimali ya dola 100 au chini ya hapo kwa sasa.
2. Gharama yako ya makazi (pamoja na gharama za matumizi ya kila siku) ni kubwa kuliko mapato yako ya kila mwezi pamoja na akiba.
3. Unafanya kazi za kilimo za msimu au za wahamiaji.

Ikiwa una ulemavu unaofanya iwe vigumu kwako kujaza au kuelewa ombi hili, tunaweza kukusaidia. Tunaweza kukupigia simu au kukutembelea ikiwa huwezi kufika ofisini kwetu. Wateja wanaweza kuwasilisha ombi la manufaa na nyenzo za uthibitishaji kwa ofisi ya kaunti yao kwa njia ya barua, kuwasilisha kwa mkono, au kutuma ombi mtandaoni kwenye <https://onedhs.tn.gov/>.

Jina (La Kwanza/La Kati/La Mwisho)			Ninatuma ombi la: ___Families First ___SNAP		
Anwani ya Nyumbani			Ikiwa una njia bora zaidi ya mawasiliano na wakati mzuri wa kukupigia simu wakati wa siku za kazi, tafadhali andika:		
Jiji	Jimbo	Msimbo wa Eneo	Simu ya Nyumbani	Simu ya Kazini	Simu ya Mkononi/Nyingine
Anwani ya Barua (ikiwa ni tofauti)			Ninaelewa kuwa ninaweza kuwa na mwakilishi mmoja au wawili walioidhinishwa:		
Jiji	Jimbo	Msimbo wa Eneo	____ anaweza kuwasilisha ombi la manufaa haya kwa niaba yangu: SNAP () ; Families First () ____ anaweza kutumia manufaa yangu ya SNAP () ; anaweza kutumia manufaa yangu ya Families First () ____ anaweza kuwasilisha ombi la manufaa haya kwa niaba yangu: SNAP () ; Families First () ____ anaweza kutumia manufaa yangu ya SNAP () ; anaweza kutumia manufaa yangu ya Families First ()		
Barua pepe:					
Je, unajiona kuwa huna makao? () Ndiyo () Hapana Je, unahitaji kadi ya EBT? () Ndiyo () Hapana		Usajili wa Wapiga Kura Je, umejiandikisha kama mpiga kura mahali unapoishi sasa? () Ndiyo () Hapana Je, ungependa kujiandikisha kama mpiga kura? () Ndiyo () Hapana Je, ungependa TDHS ikutumie fomu ya kujisajili kama mpiga kura? () Ndiyo () Hapana			
Je, unahitaji mkalimani? () Ndiyo () Hapana Je, una ulemavu au kizuizi cha lugha kinachohitaji marekebisho? () Ndiyo () Hapana		Manufaa unayoweza kupokea kutoka kwa TDHS hayatabadilika ikiwa utajiandikisha kama mpiga kura au la wala haitakuzuia kutuma maombi ya manufaa.			
Ninathibitisha chini ya adhabu ya kutoa ushahidi wa uongo (kutoa taarifa za uwongo chini ya kiapo) na adhabu zingine zote zinazotumika kuwa taarifa nilizotoa kwenye ombi hili, viambatisho vyovyote, na kwa yeyote aliyenihoji ni za kweli na sahihi. Watu wote wanaotuma ombi au wanaopokea usaidizi ni raia wa Marekani, wageni halali, au wahamiaji wanaostahiki. Ninaelewa na kukubaliana na sheria na maelezo niliyopewa. Nikiulizwa, nitatoa maelezo ambayo yanathibitisha maelezo yangu, au nitatoa ruhusa kwa TDHS kupata uthibitisho. Ninaelewa kuwa lazima niripoti mabadiliko yoyote jinsi TDHS inavyonielekeza. Ninaelewa kuwa maelezo nitakayotoa yatathibitishwa na maafisa wa serikali kuu, jimbo na serikali za mitaa ili kubaini ikiwa maelezo hayo ni ya kweli. Ondoleo la Wajibu: Jimbo la Tennessee au watu wanaolifanyia kazi wanaweza kuhitaji kuthibitisha ikiwa maelezo niliyotoa ni ya kweli. Kwa kusaini karatasi hii, ninasema kuwa ni SAWA kwao kupata uthibitisho. Hii itawawezesha kuamua ikiwa ninaweza kupata manufaa ya SNAP au Families First. Ninasema pia kuwa nimesoma na kuelewa Taarifa ya Uelewa. Ukituma ombi la SNAP, unaweza kufanyiwa ukaguzi wa Udhidhi wa Ubora. Wateja wanaweza kuwasilisha ombi la manufaa na nyenzo za uthibitishaji kwa ofisi ya kaunti yao kwa njia ya barua, kuwasilisha kwa mkono, au kutuma ombi mtandaoni katika https://OneDHS.tn.gov/.					
Saini: _____ Tarehe: _____ Shahidi (ikiwa imesainiwa kwa X): _____ Tarehe: _____					
Mlezi au Mwakilishi Aliyeidhinishwa: _____ Tarehe: _____					

Wafanyakazi wa TDHS wanapaswa kuangalia sehemu ya “Fomu” ya intraneti ili kuhakikisha matumizi ya matoleo ya sasa. Fomu haziwezi kubadilishwa bila idhini ya awali.

Tarehe ya Ukaguzi wa Mwisho:

Tarehe ya Ukaguzi Unaofuata:

HS-0169

Tarehe ya Kuanza Kutumika:

RDA: 1716

Ukurasa wa 1 kati ya 5

Tunatumia Nambari za Usalama wa Kijamii kuthibitisha utambulisho wako. Tunazitumia kuhakikisha kuwa unapata kiasi kinachofaa cha usaidizi, kubadilisha kiasi cha usaidizi unaopata, kuangalia rekodi zingine za kompyuta na serikali, na kuhakikisha kuwa unahitimu. Tunaangalia Usalama wa Kijamii, IRS, na rekodi za ajira. Tunaweza kuangalia rekodi za Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani (USCIS). Ikiwa rekodi hizo hazilingani na unachosema, inaweza kuathiri ikiwa unaweza kupata usaidizi na kiasi cha manufaa ya Families First au SNAP unayopata. Ikiwa utatoa maelezo yasiyo sahihi kwa makusudi ili kupata usaidizi, unaweza kupungwa jela.

Kwa kutoa maelezo ya Rangi/Kabila, yanasaidia kuonyesha ikiwa Tennessee linafuata sheria za haki za kiraia. Tafadhali tumia herufi zifuatazo kuashiria rangi: **W** = Mzungu, **B** = Mweusi/Mwafrika Mmarekani, **A** = Mwasia, **H** = Mzawa wa Hawaii/Visiwa Vingine vya Pasifiki, **I** = Muhindi Mmarekani/Mzawa wa Alaska (**Kaya yako haitakiwi kutupa maelezo haya na hayataathiri ustahiki wako au kiwango cha manufaa.**)

Hali ya Ndoa: Tumia mojawapo ya yafuatayo hapa chini kwa kila mwanakaya mzima: **aliyeoa/aliyeolewa, ambaye hajaoa/kuolewa, aliyetalikiwa, mjane, aliyetengana**

[illegible]

Hatia za Serikali Kuu na/au Jimbo:

Je, wewe au mtu yeyote katika kaya yako amepatikaria na hatia ya kupokea TANF (manufaa ya pesa taslimu) au manufaa ya SNAP kutoka majimbo mawili au zaidi kwa wakati mmoja? () Ndiyo () Hapana

Je, kuna mtu yeyote ambaye ametumia fedha za TANF katika sehemu zifuatazo: maduka ya vileo, kasino, vyumba vya kucheza kamari, biashara ya ngono, kumbi za bingo, barabara za mashindano ya mbio na/au maduka ya rejareja yaliyo na leseni ambayo yanapata mauzo yao makubwa kutokana na tumbaku, sigara, sigareti, mabomba na vifaa vingine vya uvutaji? (TANF pekee) Ndiyo () Hapana

Je, wewe au mwanakaya yeyote amehukumiwa kwa kununua au kuuza manufaa ya SNAP ya zaidi ya dola 500? () Ndiyo () Hapana

Je, wewe au mtu yeyote katika kaya yako ana hatia ya uhalifu wa jinai kutokana na tabia inayohusiana na umiliki, matumizi au usambazaji wa dutu ya dawa inayodhibitiwa baada ya 08/22/96 (SNAP na TANF)? () Ndiyo () Hapana

Je, wewe au mwanakaya yeyote anajificha au kukimbia kutoka kwa sheria ili kukwepa kufunguliwa mashtaka, kutiwa mbaroni, au kufungwa jela, kwa hatia ya uhalifu wa jinai au jaribio la uhalifu, au anaweza kuwa na mashtaka hayo, au hazingatii masharti ya kuachiliwa kutoka jela au uangalizi? () Ndiyo () Hapana

Je, wewe au mwanakaya yeyote amehukumiwa kwa kufanya biashara na manufaa ya SNAP kwa dawa za kulevya au dutu inayodhibitiwa? () Ndiyo () Hapana

Je, kuna mtu yeyote unayemwasilishia ombi ambaye amepokea SNAP na TANF kutoka jimbo lingine ndani ya siku 30 zilizopita? () Ndiyo () Hapana

Je, wewe au mwanakaya yeyote amehukumiwa kama mtu mzima kwa unyanyasaji wa kingono, mauaji, unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji mwingine wa watoto, kosa la Serikali kuu au Jimbo linalohusisha unyanyasaji wa kingono, au kosa chini ya sheria ya Jimbo lililobainishwa na Mwanasheria Mkuu kuwa linafanana kwa kiasi kikubwa na kosa kama hilo, baada ya tarehe 7 Februari, 2014? () Ndiyo () Hapana

KISANDUKU HIKI ni cha Families First pekee: Ruhusa ya kutoa rekodi za mahudhurio ya shule Mimi (mteja) natoa ruhusa kwa Idara ya Elimu ya Tennessee au shule ya mtoto wangu kutoa rekodi za mahudhurio ya shule ya watoto walio kwenye mpango huu kwa Tennessee Department of Human Services (Idara ya Huduma za Binadamu ya Tennessee). Idara ya Huduma za Binadamu itatumia rekodi hizi, ikiwa ni pamoja na nambari za usalama wa kijamii, kunisaidia kutimiza majukumu yangu ya Families First. Rekodi zitaharibiwa wakati hazihitajiki tena.	Maelezo yangu yatashirikiwa na Books from Birth isipokuwa ikiwa nitakataa. Alamisha hapa ili kukataa ____. Je, uko tayari kutii uamuzi wa pesa za kulea watoto? (FF Pekee) Ndiyo ____ Hapana ____	Je, ungependa kupata nakala ya ombi lako lililokamilishwa? ____Ndiyo ____ Hapana Ikiwa ndivyo, je, ungependa kupata nakala ya karatasi au ya kielektroniki? ____Nakala ya Karatasi ____Nakala ya Kielektroniki	Manufaa yako ya SNAP yanaweza kuacha kutolewa ikiwa: • Utatoa maelezo yasiyo sahihi au ufiche ukweli ili kupata manufaa ya SNAP; • Utatumia Kadi ya Usalama ya Manufaa ya mtu mwingine bila idhini yake; • Utatumia manufaa ya SNAP kununua vitu kama vile bia, sigara au sabuni au ulipe kwenye akaunti za mkopo. Ukivunja sheria hizi, hutapata manufaa ya SNAP kwa: • Mwaka 1 kwa mara ya kwanza • Miaka 2 kwa mara ya pili • Milele kwa mara ya tatu. Ikiwa utabadilisha manufaa ya SNAP kwa dawa za kulevya. Unaweza kunyimwa manufaa kwa: • Miaka 2 kwa mara ya kwanza na milele kwa mara ya pili.
Saini: _____ Tarehe: _____ Mwanakaya yeyote anayekiuka sheria yoyote kwa makusudi anaweza kuzuiwa kupata manufaa ya SNAP kwa mwaka mmoja hadi milele, kutozwa faini ya hadi dola 250,000, kufungwa kwa hadi miaka 20 au adhabu zote mbili. Anaweza pia kushtakiwa chini ya sheria zingine zinazotumika za Serikali Kuu ya Jamii. Anaweza kuzuiwa kupokea SNAP kwa miezi 18 zaidi ikiwa mahakama itaamuru. Usifanye biashara au kuzaa kadi za EBT au kutumia kadi ya mtu mwingine.			

Wafanyakazi wa TDHS wanapaswa kuangalia sehemu ya "Fomu" ya intraneti ili kuhakikisha kuwa wanatumia matoleo ya sasa. Fomu haziwezi kubadilishwa bila idhini ya awali.

Tarehe ya Ukaguzi wa Mwisho:

Tarehe ya Ukaguzi Unaofuata:

HS-0169

Tarehe ya Kuanza Kutumika:

RDA: 1716

Ukurasa wa 2 kati ya 5

Weka maelezo kuhusu MAPATO ya kaya yako katika visanduku vilivyo hapa chini. Mapato yanajumuisha lakini sio tu mapato ya kuajiriwa, kujiajiri, fedha zinazotokana na talaka, fedha za kulea watoto, manufaa ya ulemavu, Usalama wa Kijamii/SSI, Fidia ya Mfanyakazi, Manufaa yanayotolewa kwa watu wasio na ajira, pensheni, posho na mapato ya riba.			Unaweza kunyimwa SNAP milele ikiwa utapatikana na hatia ya: - Kuuza manufaa ya SNAP ili kununua bunduki, risasi, au vilipuzi au dutu zinazodhibitiwa (dawa haramu); - Kuuza manufaa ya SNAP yenye thamani ya dola 500 au zaidi. Usitoe maelezo yasiyo sahihi kukuhusu au unapoishi ili kupokea manufaa mengi ya SNAP. Kutoa maelezo yasiyo sahihi kunaweza kukuzuia kupata manufaa ya SNAP kwa miaka 10.	
Mtu mwenye Mapato kodi/gharama	Chanzo cha mapato (kama vile kazi, Usalama wa Kijamii, pesa za kulea watoto)	Kiasi cha kila mwezi kabla ya kodi/gharama		
Orodhesha Rasilimali zozote za kaya (pesa taslimu, hundi, akiba, au akaunti zingine za benki, vyeti vya amana, hisa, bondi, fedha za pamoja, akaunti za kustaafu, fedha za amana, malipo ya mwaka, au mali zinginezo zilizozwa kwa pesa taslimu) Aina: _____ Thamani:Dola _____ Aina: _____ Thamani:Dola _____ Aina: _____ Thamani:Dola _____ Aina: _____ Thamani:Dola _____				
Je, kuna mtu yeyote kati ya miaka 18 hadi 24, na amewahi kuwa chini ya ulinzi wa jimbo akiwa mtoto? () Ndiyo () Hapana	Gharama za Makazi Kodi / Rehani (chorea mduara jibu moja) Kiasi cha kila mwezi: Dola _____ Gesi/Umeme Dola _____ kwa mwezi Simu Dola _____ kwa mwezi		Gharama za Matibabu Orodhesha gharama za matibabu zinazojirudia kama vile dawa zilizoagizwa na daktari au malipo ya bima. Hizi zinaweza kukusaidia kupata manufaa zaidi ya SNAP ikiwa wewe ni mzee au mlemavu. Aina: _____ dola _____ kwa mwezi Aina: _____ dola _____ kwa mwezi	Pesa za Kulea Watoto Ikiwa una wajibu wa kisheria <u>kulipa</u> malipo ya kulea watoto kwa ajili ya mtoto au watoto andika hapa: Mtoto: _____ dola _____ kwa mwezi Mtoto: _____ dola _____ kwa mwezi
Gharama za Utunzaji wa Watoto Kiasi unacholipa kwa wiki: Dola _____ Jina la mtoa huduma ya watoto: _____				

Wafanyakazi wa TDHS wanapaswa kuangalia sehemu ya “Fomu” ya intraneti ili kuhakikisha kuwa wanatumia matoleo ya sasa. Fomu haziwezi kubadilishwa bila idhini ya awali.

Tarehe ya Ukaguzi wa Mwisho:

Tarehe ya Ukaguzi Unaofuata:

HS-0169

Tarehe ya Kuanza Kutumika:

RDA: 1716

Ukurasa wa 3 kati ya 5

Taarifa ya SNAP na FDPIR ya Kutobagua ya Fomu ya Pamoja ya Kutuma Maombi

Kwa mujibu wa sheria za Serikali za haki za kiraia na kanuni na sera za haki za kiraia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), USDA, mashirika yake, ofisi na wafanyakazi wake, na taasisi zinazoshiriki au kusimamia programu za USDA haziruhusiwi kubagua kwa misingi ya rangi, asili ya kitaifa, jinsia (ikijumuisha utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia), imani ya kidini, ulemavu, umri, imani za kisiasa, au kulipiza kisasi au kulipiza kisasi kwa sababu ya shughuli za awali za haki za kiraia katika programu au shughuli yoyote inayoendeshwa au kufadhiliwa na USDA. Programu zinazopokea usaidizi wa kifedha wa Serikali kutoka kwa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Marekani (HHS), kama vile Usaidizi wa Muda kwa Familia Zilizoa Uhitaji (TANF), na programu zinazoendeshwa na HHS moja kwa moja pia haziruhusiwi kubagua chini ya sheria za Serikali za haki za kiraia na kanuni za HHS.

Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano ya maelezo ya programu (k.m., Breli, maandishi makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani), wanapaswa kuwasiliana na wakala wa (jimbo au eneo) ambako walituma maombi ya udhamini. Watu ambao ni viziwi, wasiosikia vizuri au wenye ulemavu wa kuzungumza wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Usambazaji ya Serikali kwa (800) 877-8339. Zaidi ya hayo, maelezo ya programu yanaweza kupatikana katika lugha nyingine isipokuwa Kiingereza.

MALALAMISHI YA HAKI ZA KIRAIA YANAYOHUSISHA PROGRAMU ZA USDA

USDA hutoa msaada wa kifedha wa Serikali kwa programu nyingi za usalama wa chakula na kupunguza njaa kama vile Programu ya Usaidizi wa Lishe ya Ziada (SNAP), Programu ya Usambazaji wa Chakula kwenye Hifadhi za Kihindi (FDPIR) na zingine. Ili kuwasilisha malalamishi ya ubaguzi ya programu, jaza Fomu ya Malalamishi ya Ubaguzi ya Programu, (AD-3027) inayopatikana mtandaoni kwa:

<https://www.fns.usda.gov/sites/default/files/resource-files/ad3027-swahili.pdf>

na katika ofisi yoyote ya USDA au andika barua kwa anwani ya USDA na utoe katika barua habari zote zilizoombwa kwenye fomu. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamishi, piga simu (866) 632-9992.

Wasilisha fomu au barua yako iliyojazwa kwa USDA kwa:

1. **Barua:** Food and Nutrition Service, USDA
1320 Braddock Place, Room 334, Alexandria, VA 22314; au
2. **faksi:** (833) 256-1665 au (202) 690-7442; au
3. **simu:** (833) 620-1071; au
4. **barua pepe:** FNSCIVILRIGHTSCOMPLAINTS@usda.gov.

Kwa taarifa nyingine yoyote kuhusu masuala ya SNAP, watu wanapaswa kupiga simu kwa Nambari ya USDA SNAP kwa (800) 221-5689, ambayo pia ni ya Kihispania, au wapige simu kwa Nambari za Taarifa za Serikali (bonyeza kiungo ili kupata orodha ya nambari za simu kwa jimbo); inayopatikana mtandaoni kwa: <https://www.fns.usda.gov/snap/state-directory>.

MALALAMISHI YA HAKI ZA KIRAIA YANAYOHUSISHA PROGRAMU ZA HHS

HHS huandaa Usaidizi wa Kifedha wa Serikali kwa programu nyingi za kuimarisha afya na ustawi, ikiwa ni pamoja na TANF, Head Start, Programu ya Usaidizi wa Nishati kwa Familia zenye Mapato ya Chini (LIHEAP), na zingine. Iwapo unaamini kuwa umebaguliwa kwa sababu ya rangi yako, asili ya taifa, ulemavu, umri, jinsia (ikiwa ni pamoja na ujauzito, mwelekeo wa ngono na utambulisho wa kijinsia), au dini katika programu au shughuli ambazo HHS inaendesha moja kwa moja au ambayo HHS huandalia

usaidizi wa kifedha wa Serikali, unaweza kuwasilisha malalamishi kwa Ofisi ya Haki za Kiraia (OCR) kwa ajili yako au mtu mwingine.

Ili kuwasilisha malalamishi ya ubaguzi kwa ajili yako au mtu mwingine kuhusu mpango unaopokea usaidizi wa kifedha wa Serikali kupitia HHS, jaza fomu mtandaoni kupitia Tovuti ya Malalamishi ya OCR kwa: <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/>. Unaweza kuwasiliana na OCR kupitia barua kwa: Centralized Case Management Operations, U.S. Department of Health and Human Services, 200 Independence Avenue, S.W., Room 509F HHH Bldg., Washington, D.C. 20201; Fax: (202) 619-3818; au barua pepe OCRmail@hhs.gov. Kwa uchakataji wa haraka, tunakuhimiza utumie sehemu ya mtandao ya OCR kuwasilisha malalamishi badala ya kuwasilisha kupitia barua. Watu wanaohitaji usaidizi wa kuwasilisha malalamishi ya haki za kiraia wanaweza kutuma barua pepe kwa OCR kwa: OCRMail@hhs.gov au kupigia OCR simu bila malipo kupitia 1-800-368-1019, TDD 1-800-537-7697. Kwa watu ambao ni viziwi, wasiosikia vizuri, au walio na matatizo ya kuzungumza, tafadhali piga 7-1-1 ili kupata huduma za mawasiliano ya simu. Pia tunatoa miundo mbadala (kama vile Breli na maandishi makubwa), vifaa vya usaidizi na huduma za usaidizi wa lugha bila malipo ili kuwasilisha malalamishi.

Taasisi hii hutoa fursa kwa usawa.